



Sehemu za Jamii

MABADILIKO KWA HUDUMA KUTOKANA NA COVID-19

Msaada chini ya Sehemu za Jamii unaendelea kupatikana kwa wateja wakati wa mlipuko wa COVID-19. Hata hivyo, njia ambayo huduma zinawasilishwa inaweza kubadilika kulingana na ushauri rasmi wa afya.

Katika maeneo mengi ya Sehemu, kumekuwa na upunguzaji wa mawasiliano ya uso kwa uso. Viongozi wa Sehemu wanaendelea mawasiliano na wateja binafsi kupitia simu. Vikao vya kikundi vitahamia mtandaoni, kuhakikisha kuwa jamii zinaendelea kuunganishwa na viongozi wa Sehemu za jamii, pamoja na kila mmoja na kuendelea kushiriki katika shughuli muhimu kama vile masomo ya Kiingereza cha kuongea.

Jifunze kuhusu **COVID-19 na dalili zake (symptoms)**.

Nini maana ya Sehemu za Jamii?

Sehemu za Jamii (pia inajulikana kama Mpango wa Taifa wa Sehemu za Jamii) ni maeneo ya kukaribishana kwa familia za wahamiaji na wakimbizi, hasa kina mama wenye watoto wadogo.

Sehemu hizo za Jamii ziko katika shule za msingi na zinasaidia watu kujifunza Kiingereza, kukuza ujuzi mpya, kupata ajira na kutoa msaada ili kusaidia kufikia huduma za msaada wa Serikali.

Sehemu za Jamii zinapatikana wapi?

- NSW: Parramatta, Blacktown, Canterbury Bankstown, Fairfield, Cumberland, Wollongong, Liverpool
- VIC: Brimbank, Dandenong, Hume, Banyule, Geelong, Shepparton
- QLD: Logan, Ipswich
- SA: Port Adelaide – Enfield, Salisbury

Orodha ya shule za msingi zinazo Sehemu za Jamii na maelezo ya mawasiliano yanaweza kupatikana [hapa](#).

Sehemu za Jamii zinatoa huduma gani?

Huduma zinazotolewa hutofautiana kati ya Sehemu za Jamii, kuhakikisha kuwa zinafikia mahitaji ya jamii yao ya ndani. Mifano ya aina ya shughuli ni kama zifuatavyo:

- Vikundi vya kuchezea na mipango ya watoto wa miaka ya kwanza
- Madarasa ya Kiingereza na mipango ya mazungumzo
- Warsha na vikundi vya maisha ya afya na vya ujuzi mengine wa maisha

- Ushiriki wa wazazi na mipango ya kujenga uwezo
- Lugha za watoto na mipango ya kusoma
- Fursa za kujitolea na msaada wa ajira
- Mafunzo ya ujuzi rasmi wa kazi kwa kushirikiana na TAFE na mashirika ya mafunzo yaliyosajiliwa
- Warsha zisizo rasmi za maendeleo ya ustadi
- Makundi ya maslahi maalum na ya kijamii
- Safari za nyanjani na kutembea kwa vikundi
- Kutoa rufaa kwa programu zingine ambazo zinaweza kusaidia katika maswala

Je ninastahili kupokea huduma?

Wahamiaji wote wanakaribishwa katika Sehemu za Jamii. Kuna kulenga kwa wahamiaji akina mama wanao watoto.

Naweza kujua zaidi namna gani kuhusu huduma za Sehemu za Jamii?

Kama ukipenda habari zaidi tembelea kwenye tovuti ya [**Community Hubs**](#) au piga simu 03 8614 3430.